إِذَا أَدْرَكَ الْإِمَامَ رَاكِعًا فَمَاذَا يَفْعَلُ؟

JE, ATAFANYA NINI YULE ALIYEMDIRIKI IMAMU YUPO KWENYE RUKUU?

Mwandishi:
Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud

Utangulizi

Kila sifa njema anastahiki Allaah Mola wa viumbe wote, na swala za Allaah na salamu zimuendee Mtume wetu, Wafuasi wake na Maswahaba wake wote.

Baada ya hayo,

Hii ni Makala fupi yenye kuelezea jambo analopasa mtu kulifanya pindi akimkuta imamu amerukuu.

Nimeandika Makala hii baada ya kuona hali za watu wengi katika misikiti niliyowahi kuswali katika maeneo tafauti, namna wanavyokosea katika swala zao hasa katika kumfuata imamu hali ya kuwa yupo katika rukuu.

Mtu akimkuta imamu amerukuu hupatikana moja kati ya mambo matatu:

1. Kuwa na uhakika kuwa amemdiriki imamu kabla hajanyanyuka, na wakati huu atakuwa ameipata rakaa hiyo.
2. Kuwa na uhakika kuwa imamu alinyanyuka kabla yeye hajarukuu, kwa hiyo rakaa hiyo ameikosa.
3. Kupata shaka, je alimdiriki imamu kabla hajanyanyuka au imamu alinyanyuka kabla yeye hajarukuu sawasawa?

Ama hali ya kwanza na ya pili jambo lao ni jepesi, isipokuwa hali ya tatu inahitaji ufafanuzi na hiyo ndiyo sababu ya kuandika Makala yetu hii, pamoja nitataja mambo mengine kuhusiana na rukuu.

Na nimeeita Makala hii: **Je, atafanya nini mtu aliyekuja msikitini akamdiriki Imamu hali ya kuwa yupo kwenye rukuu?.**

Namuomba Allaah anijaalie Ikhlaas na Taufiq katika amali yangu hii, kama ninavyomuomba (Allaah) aniruzuku elimu yenye manufaa mimi na ndugu zangu waislamu, na aturuzuku mwisho mwema.
Na Allaah amsifie Mtume wetu Muhammad, wafuasi wake na Maswahaba wake wote na awape Amani.

Abu Halima Arafaat.

بسم الله الرحمن الرحيم

Nukta ya Kwanza: Nini maana ya rukuu?:

Maana ya rukuu katika lugha ya kiarabu ni kunyenyekea.

Na katika maana ya sheria ni kama alivyosema imam Al-Qurtubi رَحِمَهُ الله :

«الرُّكُوعُ الشَّرْعِيُّ هُوَ أَنْ يَحْنِيَ الرَّجُلُ صُلْبَهُ وَيَمُدَّ ظَهْرَهُ وَعُنُقَهُ وَيَفْتَحَ أَصَابِعَ يَدَيْهِ وَيَقْبِضَ عَلَى رُكْبَتَيْهِ ثُمَّ يَطْمَئِنَّ رَاكِعًا»

[Rukuu ya kisheria ni kuwa mtu akunje uti wa mgongo wake, na aunyooshe mgongo wake na shingo yake, na atenganishe vidole vya mikono yake na akamate magoti yake, kisha atulizane hali ya kuwa amerukuu][1].

Nukta ya Pili: Itamtosheleza yeye kusoma Takbira moja tu (ya kuhirimia):

Ikiwa mtu amekuja msikitni akamkuta imamu amerukuu, itamtosheleza yeye kusoma takbira moja tu ya kuhirimia, kisha atarukuu, wala si wajibu kwake kusoma takbira ya kwenda kwenye rukuu.

Aliulizwa sheikh Ibn Baaz رَحِمَهُ اللهُ kuhusu maamuma aliyemkuta imamu katika rukuu, je atasoma takbira moja tu ya kuhirimia au zote mbili?

Akajibu:

«الأَوْلَى وَالْأَحْوَطُ أَنْ يُكَبِّرَ التَّكْبِيْرَتَيْنِ: إِحْدَاهُمَا: تَكْبِيْرَةُ الْإِحْرَامِ، وَهِيَ رُكْنٌ وَلَا بُدَّ أَنْ يَأْتِيَ بِهَا وَهُوَ قَائِمٌ، وَالثَّانِيَةُ: تَكْبِيْرَةُ الرُّكُوْعِ يَأْتِيْ بِهَا حِيْنَ هُوِيِّهِ إِلَى الرُّكُوْعِ فَإِنْ خَافَ فَوْتَ الرَّكْعَةِ أَجْزَأَتْهُ تَكْبِيْرَةُ الإِحْرَامِ فِي أَصَحِّ قَوْلَيِ العُلَمَاءِ».

[Lliyo bora na kujitoa katika shaka ni kuwa asome takbira zote mbili: <u>Ya kwanza</u> ni takbira ya kuhirimia, nayo ni nguzo katika swala, na ailete hali ya kuwa amesimama. <u>Ya pili</u> ni takbira ya kurukuu, ataileta wakati wa kupinda kwenda kwenye rukuu, lakini akihofia kuikosa rakaa hiyo (kwa kunyanyuka imamu kabla yeye hajarukuu) basi itamtosheleza yeye takbira (moja tu) ya kuhirimia katika kauli iliyo sahihi zaidi miongoni mwa kauli mbili za Maulamaa][2].

1- Tazama kitabu: [Tafsiirul Qurtubi] (Jz. 1, Uk. 345).

2- Tazama kitabu: [Majmuu' fataawa Ibn Baaz] (Jz. 11, Uk. 244-245).

Nukta ya Tatu: Inampasa asome Takbira ya kuhirimia akiwa amesimama

Amesema Imam Nnawawi رَحِمَهُ اللهُ :

«إِذَا أَدْرَكَ الْإِمَامَ رَاكِعًا كَبَّرَ لِلْإِحْرَامِ قَائِمًا ثُمَّ يُكَبِّرُ لِلرُّكُوعِ وَيَهْوِي إِلَيْهِ فَإِنْ وَقَعَ بَعْضُ تَكْبِيرَةِ الْإِحْرَامِ فِي غَيْرِ الْقِيَامِ لَمْ تَنْعَقِدْ صَلَاتُهُ فَرْضًا بِلَا خِلَافٍ وَلَا تَنْعَقِدُ نَفْلًا أَيْضًا عَلَى الصَّحِيحِ»

[Akimdiriki imamu katika rukuu atasoma takbira ya kuhirimia hali ya kuwa amesimama, kisha atasoma takbira ya rukuu na atapinda kurukuu, ikiwa baadhi ya (matamko) ya takbira ya kuhirimia yalipatikana (alitamka) katika isiyokuwa kisimamo, basi swala yake ya faradhi itakuwa haijatungika bila ya khilafu yoyote, na pia swala ya sunnah juu ya kauli iliyo sahihi[3]][4].

Ndio maana sheikh Uthaymin akalihimiza jambo hilo, akasema:

«وَلَكِنْ هُنَا أَمْرٌ يَجِبُ أَنْ يُتَفَطَّنَ لَهُ، وَهُوَ أَنَّهُ لَا بُدَّ أَنْ يُكَبِّرَ لِلْإِحْرَامِ قَائِمًا مُنْتَصِبًا قَبْلَ أَنْ يَهْوِيَ؛ لِأَنَّهُ لَوْ هَوَى فِيْ حَالِ التَّكْبِيْرِ لَكَانَ قَدْ أَتَى بِتَكْبِيْرَةِ الإِحْرَامِ غَيْرَ قَائِمٍ وَتَكْبِيْرَةُ الإِحْرَامِ لَا بُدَّ أَنْ يَكُوْنَ فِيْهَا قَائِمًا»

[Lakini hapa kuna jambo ambalo linapasa kufahamika, nalo ni kwamba lazima asome takbira ya kuhirimia akiwa amesimama wima kabla hajapinda (kurukuu); kwa sababu lau alirukuu wakati akisoma takbira ya kuhirimia, atakuwa ameileta takbira hiyo pasi na kusimama, na takbira ya kuhirimia ndani ya swala lazima aisome akiwa amesimama][5].

Nukta ya Nne: Ni wakati gani atazingatiwa amemdiriki imamu katika rukuu?

Endapo mtu amemdiriki Imamu katika rukuu, atamfuata na atazingatiwa kuwa ameidiriki rakaa hiyo, ikiwa alimpata Imamu kwenye rukuu kabla hajanyanyuka, hata kama imamu alinyanyuka kabla yeye hajatulizana sawasawa.

Amesema Imam Abu Daud رَحِمَهُ اللهُ :

«سَمِعْتُ أَحْمَدَ، سُئِلَ عَمَّنْ أَدْرَكَ الْإِمَامَ رَاكِعًا فَكَبَّرَ، ثُمَّ رَكَعَ فَرَفَعَ الْإِمَامُ؟ قَالَ: إِذَا أَمْكَنَ يَدَيْهِ مِنْ رُكْبَتَيْهِ قَبْلَ أَنْ يَرْفَعَ الْإِمَامُ فَقَدْ أَدْرَكَ»

---

[3]- Ikiwa alisoma baadhi ya maneno ya takbira mfano: **(Allaahu Akbar)** akiwa amesimama, na neno **(Akbar)** alisema wakati amepinda mgongo wake kwenda kwenye rukuu, basi swala yake haitasihi.

[4]- Tazama kitabu: [Al-Majmuu'] (Jz. 1, Uk. 213).

[5]- Tazama kitabu: [As Sharhul Mumti'] (Jz. 4, Uk. 170).

[Nimemsikia Imam Ahmad akiulizwa kuhusiana na (mtu) aliyemdiriki imamu katika rukuu, naye akapiga takbira (akamfuata imamu) katika rukuu, (lakini) imamu akawa amenyanyuka. Amesema (imamu Ahmad): Akiwa aliweka mikono yake katika magoti yake kabla imamu hajanyanyuka, atakuwa amemdiriki][6].

Amesema Sheikh Ibn Baaz رَحِمَهُ اللهُ akifafanua namna ya kuidiriki rakaa:

«إِذَا أَدْرَكَ المَأْمُوْمُ الإِمَامَ رَاكِعًا أَجْزَأَتْهُ الرَّكْعَةُ وَلَوْ لَمْ يُسَبِّحِ المَأْمُوْمُ إِلَّا بَعْدَ رَفْعِ الْإِمَامِ».

[Ikiwa maamuma atamdiriki imamu katika rukuu basi itamtosheleza yeye rakaa hiyo (atazingatiwa ameipata) hata kama hakusema (Subhaana Rabbiyal 'Adhiim) isipokuwa baada ya kunyanyuka imamu][7].

Ushahidi ni hadithi ya Mtume ﷺ inayosema:

«مَنْ أَدْرَكَ الرُّكُوعَ فَقَدْ أَدْرَكَ الرَّكْعَةَ»

[Mwenye kuidiriki rukuu basi amediriki rakaa kamili)][8].

Nukta ya Tano: Si wajibu kwake katika hali hiyo kusoma Surat Al-Faatiha

Zimekuja hadithi mbalimbali zinazoelezea uwajibu wa kusoma surat Al-faatiha ndani ya swala, na kwamba jambo hilo ni wajibu juu ya kila mwenye kuswali, ni sawa alikuwa imamu, maamuma, au mwenye kuswali peke yake, lakini kuna hadithi iliyokuja kuhusisha kwa mtu aliyemkuta imamu amerukuu, kwamba mtu huyo hatasoma surat Al-faatiha.

عَنْ أَبِي بَكْرَةَ، أَنَّهُ انْتَهَى إِلَى النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَهُوَ رَاكِعٌ، فَرَكَعَ قَبْلَ أَنْ يَصِلَ إِلَى الصَّفِّ، فَذَكَرَ ذَلِكَ لِلنَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقَالَ: «زَادَكَ اللَّهُ حِرْصًا وَلاَ تَعُدْ»

"Imepokewa kutoka kwa Abu Bakra رَضِيَ اللهُ عَنْهُ , kwamba yeye alifika kwa Mtume ﷺ na hali ya kuwa yeye amerukuu, (naye) akarukuu kabla hajafika kwenye safu[9], kisha akamsimulia hilo Mtume ﷺ, akasema: [Allaah akuzidishie pupa na wala usirudie tena][10].

6- Tazama kitabu: [Masaailul imam Ahmad Li-Abi Daud] (Uk. 53).
7- Tazama kitabu: [Majmuu Fataawa Ibn Baaz] (Jz. 11, Uk. 245-246).
8- Tazama kitabu: [Ir-waaul ghaliil] (Uk. 496).
9- Alipoingia msikitini alimkuta Mtume ﷺ amerukuu, akaona lau kama alitembea mpaka kwenye safu Mtume ﷺ atanyanyuka, akaamua arukuu kabla ya kufika kwenye safu kisha akatembea hali ya kuwa amerukuu mpaka akaingia kwenye safu, Mtume ﷺ hakumgombeza kwa jambo hilo wala hakumuamrisha kurudia upya swala yake; ikajulisha kwamba si wajibu kwake surat Al-Faatiha.
10- Tazama kitabu: [Sahihil Bukhari] (783).

Na njia ya kutolea ushahidi kwa hadithi hiyo ni kwamba, lau ingelikuwa kumdiriki kwake imamu katika rukuu hakutoshelezi kuwa ameidiriki rakaa hiyo pamoja imamu, basi Mtume ﷺ angemuamrisha kuirudia rakaa hiyo, na pia hakusoma ndani yake suratul Faatiha, kwa hiyo hadithi hii inafahamisha kwamba mwenye kuidiriki rukuu ameidiriki rakaa.

Muhtasari wa yaliyotangulia:

Akiwa mtu amemdiriki imamu katika rukuu, kwanza anatakiwa asome Takbira ya kuhirimia (takbiiratul Ihraam) yote hali ya kuwa amesimama, wala asipinde mgongo wake kurukuu isipokuwa baada ya kumaliza kusoma Takbiiratu Ihraam. Na atazingatiwa amemdiriki imamu katika rukuu ikiwa ataweka mikono yake kwenye magoti yake kabla imamu hajanyanyuka, hata kama imamu alinyanyuka kabla yeye hajaanza kusoma adhkaar za rukuu (subhaana Rabbial 'Adhim n.k), na wakati huo atazingatiwa ameipata rakaa hiyo pamoja na imamu. Na wala si wajibu kwake katika hali hiyo kusoma surat Al-faatiha.

Nukta ya Sita: Je atafanya nini yule aliyepata shaka katika rukuu yake?

Sehemu hii nitalitaja jambo muhimu sana ambalo anapasa kulijua kila mwenye kuswali, na watu wengi wanakosea kwa sababu hawajui nini afanye mtu akipatwa na jambo hili Namuomba Allaah aniwezeshe kufafanua kiasi cha kuelewa kila atakaesoma Makala yetu hii.

Mfano, mtu ameingia msikitini amempata imamu amerukuu, akasoma takbira ya kuhirimia kisha akarukuu, akiwa katika hali hiyo akapata shaka; **je alimdiriki imamu katika rukuu kabla hajanyanyuka au imamu alinyanyuka kabla yeye hajaweka mikono yake juu ya magoti yake?.**

Hatua ya kwanza atafute usahihi, atafakari na kurudisha kumbukumbu zake vizuri, lile ambalo litapata nguvu katika akili yake atalifanyia kazi, kwa hiyo ima litapata nguvu kuwa amempata au litapata nguvu kinyume chake (hakumpata), katika hali zote hizi mbili ataleta sijda ya kusahau baada ya kutoa salamu, kwa sababu ya hadithi inayosema: **[Akipata shaka mmoja wenu katika swala na atafute usahihi, kisha akamilishe swala yake na atoe salamu, kisha asujudu sijda mbili (za kusahau)]**[(11)].

[11]- Bukhari: (401), Muslim: (89).

Na ikiwa amepata shaka, lakini hakupata lenye nguvu katika dhana yake, basi atarudi kwenye yakini, nayo ni kuwa hakumdiriki imamu, kwa sababu asili ni kuwa yeye hakuanza na imamu tangu mwanzo wa swala yake, kwa hiyo rakaa hiyo hataihesabu, na badala yake ataleta rakaa kamili baada imamu kutoa salamu, kisha ataleta sijda ya kusahau kabla ya kutoa salamu wakati akikamilisha swala yake, kwa sababu ya hadithi inayosema: **[Akipata shaka mmoja wenu katika swala yake na akawa hajui ni rakaa ngapi ameswali, tatu au nne? Basi aiache shaka na ajengee kwenye yakini, kisha asujudu sijda mbili kabla ya kutoa salamu].**

Je, ni ipi faida ya kuleta sijda ya kusahau baada ya kurudi kwenye yakini?

Hadithi iliyotangulia imetaja kuwa mtu ataleta sijda mbili za kusahau, pale atakapojengea juu ya yakini, na faida ya kuleta sijda hizi ni kama ilivyotajwa mwishoni mwa hadithi hiyo: **[kama atakuwa ameswali rakaa tano (basi sijda hiyo) itamsawazishia yeye swala yake, na kama alitimiza rakaa nne itakuwa ni kwa ajili ya kumchukiza shetani]**[(12)].

Namna ya kutolea ushahidi katika hadithi hii ni kwamba, mtu huyo amerudi kwenye yakini baada ya kuwa amepata shaka na kutojua ni lipi limepatikana (je alimpata imamu katika rukuu au alimkosa), na miongoni mwa sababu zinazopelekea kuleta sijda ya kusahau ni mtu kupata shaka, kwa hiyo baada ya kuwa ameleta rakaa moja kwa ajili ya kutimiza swala yake ni wajibu wake kuleta ya kusahau ili kufuta shaka iliyozuka katika swala yake, **ikiwa alimdiriki imamu kwenye rukuu basi sijda hiyo itamsawazishia yeye swala yake (itaifuta ile rakaa moja iliyozidi), na kama alimkosa (imamu alinyanyuka kabla yeye hajaweka mikono kwenye magoti yake) basi itakuwa ni kwa ajili ya kumchukiza shetani.**

Wabillaahi Ttaufiq

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud
1/rabiiul Aakhar/1444ᴴ – 26/10/2022ᴹ
Pongwe Tanga
Tanzania.

[12]- Muslim: (88).